MINISTRY OF EDUCATION

# KCSE 2023 REGIONAL MOCKS

# KISWAHILI

THE PDF COMPRISES A COMPILATION OF TOP 4 JOINT NATIONAL MOCKS ACROSS THE 47 COUNTIES FOR THE KCSE CLASS OF 2023

REPUBLIC OF KENYA
MINISTRY OF EDUCATION


## FOR MARKING SCHEMES:

## CONTACT:

## MR MACHUKI – 0724333200

## OR

## ORDER ONLINE AT:

## *www.kenyaeducators.co.ke*

**KENYA EDUCATORS CONSULTANCY**



Compiled and Distributed by Kenya Educators Consultancy, P.O.BOX 15400-00500, Nairobi.
Tel 0724333200 E-mail kenyaeducators@gmail.com. ORDER MARKING SCHEMES & SIMILAR RESOURCES AT www.kenyaeducators.co.ke or Contact 0724333200/0768321553/0795491185

# TABLE OF CONTENTS:


| | |
|---|---|
| 1. | THE NAIROBI & CENTRAL REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023 |
| 2. | THE NYANZA & WESTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCKS 2023 |
| 3. | THE COASTAL & EASTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023 |
| 4. | THE RIFT VALLEY & NORTH EASTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023 |


## CONFIDENTIAL!!!

## SUCCESS TO ALL KCSE 2023 CANDIDATES!!!

**Jina……………………………………Nambari ya Usajili………………..Darasa………**

**Tarehe ………………………………………Sahihi ya mtahiniwa……………………**

**102/1**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 1**

**KIDATO CHA NNE**

# THE NAIROBI & CENTRAL REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023

**MAAGIZO**

a) *Andika jina lako na nambari ya usajili kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima.***
d) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
e) *Kila insha isipungue maneno **400**.*
f) *Kila insha ina alama **20.***
g) *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya **Kiswahili.***
h) *Insha zote sharti ziandikwe katika nafasi ulizoachiwa kwenye kijitabu hiki cha maswali.*
i) *Karatasi hii ina kurasa **8** zilizopigwa chapa.*
j) *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

 ©2023 The Kenya National Examinations Council 
Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes

1. **LAZIMA**
   Chamko la ugonjwa wa Korona lililemaza shughuli za michezo nchini. Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa na Waziri wa Michezo kubuni mikakati ya kufufua michezo katika taasisi za elimu nchini. Andika kumbukumbu za mkutano huo.

2. Vijana wamekuwa wakichelea kuhusika katika mchakato wa uchaguzi. Jadili vyanzo vya hali hii huku ukiwapendekezea vijana umuhimu wa kubadili msimamo huu.

3. Tunga Kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.

4. Andika insha itakayomalizikia kwa:
   *...nilipotua nchini, nilishusha pumzi, nikamshukuru Jalia kwa kuponea chupuchupu katika uvamizi huo.*

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………


*Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes*

..........................................................................................................................................

..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................
..................................................................................................................................

*Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes*

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………....................................……………………………………...

**MINISTRY OF EDUCATION (KNEC COMPLIANT)**

**JINA……………………………………………………NAMBARI YAKO…………..**

**SAHIHI…………………DARASA…………………… TAREHE…………………**

**KISWAHILI –**
**KARATASI YA 2**
**Muda : Saa 2**

# THE NAIROBI & CENTRAL REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023

**MAAGIZO**

- Jibu maswali **yote** katika nafasi ulizopewa**.**
- Majibu lazima yaandikwe katika lugha ya Kiswahili
- Usitoe ukurasa wowote katika kijitabu hiki.
- Kila mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote zimepigwa chapa pamoja na maswali.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI :**

| | **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|---|
| **1.** | **UFAHAMU** | 15 | |
| 2. | UFUPISHO | 15 | |
| 3. | SARUFI | 40 | |
| 4. | ISIMUJAMII | 10 | |
| | **JUMLA** | **80** | |

1. **UFAHAMU** ***( Alama 15)***

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.**

Kijiji cha Mulukoba kilikuwa na utulivu wa aina yake. Okolo alikuwa miongoni mwa wazaliwa wa eneo hilo. Katika miaka ya tisini alikuwa ameanza safari yake ya masomo katika Shule ya Msingi ya Magombe.Enzi hizo mshawasha na imani za watu zilihusu tu maswala ya elimu.

Okolo alifurahishwa na utangamano wa kijiji chao. Watu walishirikiana kazini, sherehe za arusi, matanga aghalabu shughuli ya mtu iligusa mwenzake. Anakumbuka vizuri ngoma zilizopigwa katika sherehe mbalimbali wanakikundi cha 'Alaki' wakiongoza ilikuwa burudani ya aina yake. Na je, baragumu lililopulizwa na Achwari kuwaita watu kununua nyama na kujuza watu kuwa fulani ameaga? Kwa kweli Mulukoba kilikuwa kijiji chenye ufanisi.

Kando na hayo, vyakula walivyokuwa navyo hasa samaki waliovuliwa mto Akanyo hususan kambare, walikuwa na ladha ya kupendeza. Okolo alifurahia sana samaki wa kukaushwa 'kerewa' namna wanakijiji walivyoita. Huyu alikuwa chaguo lake, mamake alipopika siku hiyo basi ukamilifu ulijaa moyoni mwake. Okolo alitumai kuwa atakapooa, basi mkewe ni sharti afahamu kuwa 'kerewa' ndicho chakula chake. Mto huu pia ulikuwa kitovu cha michezo ya kitoto, ulikuwa na vivukio vitatu, kwa Alaki, kwa Nikola na Bobobo. Kidimbwi kizuri cha kupiga binzi kilikuwa kivukio cha Nikola. Vivukio hivi viliitwa majina haya kutokana na mwenye ardhi palipo kivukio hicho. Mazingira ya pale pia yalimpendeza. Hili humfanya akumbuke hadithi aliyosoma chuo kikuu ya E. Kezilahabi kuhusu Mayai Waziri wa Maradhi wakiogelea mtoni. Enzi hizo za miaka ya tisini mwanzo mtu hakujisumbua na lazima lazima za sabuni. Mradi umeona maji, kulikuwa na mawe ya kusugua mguu pale mtoni, wengine wangetumia mchanga nayo sabuni ilikuwa harita au matawi ya mti walioita 'sabuni ya wazee'. Yaani wakati huo binadamu alitumia mali asili kwenye shughuli zake za kila siku.Leo hii anapojitia marashi na hata mkewe kumkumbusha aina za sabuni nzuri, hucheka pasi yeyote kutambua kiini cha kicheko hicho.

Je, ukarimu nao wa wanakijiji. Enzi hizo watu walisaidiana. Anakumbuka babake akiwaalika wanakijiji katika sherehe tu za burudani. Atoka mchezo tiriri akiongoza burudani huku wengine wakila na kunywa. Bangaradesi mmoja wa wanakijiji angecheza wimbo wa Atoka kwa miondiko yote. Huo ndio ukamilifu uliokuwepo. Anakumbuka wagema wawili waliofahamika sana , Akong'o na Majimaji. Majimaji alikuwa rafiki wa dhati wa babake, kila mara babake angetaka kuonja kinywaji, Okolo angeshika njia hadi kwake. Pombe aliyoenzi sana babake ni 'chang'aa. Akongo alikuwa mmoja wa wagema wapenzi wa babake, alipotumwa kununua pombe, kila mara Akongo angempa kiasi kwenye gilasi kama mbinu ya kumkumbusha ukamilifu wa mwanamume Mulukoba kwani waliokosa kunywa pombe walionekana wanyonge katika jamii. Ukweli ni kuwa Okolo alionja pombe zote, hata zingine kubugia, lililompiga mshipa kila mara ni habari ingewafikia walimu wake, hilo tu lingempa kwaheri ya masomo.

Katika shughuli hizi zote, Okolo alishauriwa na mamake kutilia maanani masomo. Ni kutokana na hali hii ukaamua kupea masomoni kwa matumaini ya kuwa kuajiriwa na vilevile kufaa kijiji chake.

Ni miaka kumi na mitano baada ya Okolo kutimiza ndoto yake. Leo hii ni mkurugenzi wa matibabu katika mojawapo wa hospitali nchini. Hatua zake za mwanzo alizofanya ni kuenda

kuwafaa wenzake na wanyonge kijijini, hususan wale waliosoma nao ambao hawakufaulu kielimu. Amefadhili wanafunzi wengi mayatima hadi shule ya upili. Ndoto yake ya kufaa kijiji chake, ule ustaarabu na ujamaa ndiyo- azma yake. Gari alilonunua angalabu humsaidia yeyote mwenye safari ya dharura au hata mgonjwa. Kwa kuwa anafanya kazi mjini, yeye hupenda kuwaletea wanawake kanga. Kwa kweli miaka mitano tu jina lake lilienea na kutawala Mulukoba na kuvuka mipaka zaidi. Japo babake ameaga, amewahi kuita kikundi cha wacheza ngoma cha 'Alaki' katika hafia ya kumkumbuka babake.
Kwa kweli, malezi aliyopata kwa misingi ya ujamaa ni tiyara inayompeperusha. Kila mara atokapo mjini, yeye husalimia angalabu kila jirani yake. Mapeni yakiwa mfukoni hakosi kumuani mwenye taabu. Lakini kwa sasa, Okolo ameanza kusadiki kisa alichosoma kwenye riwaya ya Said Ahmed ya utengano kuwa hakuwa kijichobadilika ila mabadiliko yenyewe. Okolo amejipata tu ni yeye anayegonga mlango ya watu kuwajulia hali. Hata majirani waliofana kama yeye hawajali. Kutia msumari kwenye kidonda ni kuwa ukarimu wake umekuwa mada ya minong'ono kijijini.

Alipotangaza kuwania udiwani hakujua kuwa ilikuwa ni mbinu ya kuchunguza ufanisi wake. Juzi amepata habari kuwa kuna baadhi ya wanaodai kuwa yeye ni mwizi wa mali ya umma, wengine wanadai ana mazingaumbwe. Ajabu ni kuwa kuna wanaodai kuwa aila yake haijawahi kuwa na kiongozi hata mzee wa kijiji, hivyo basi hana nafasi pale. Kinachomkata maini zaidi ni kuna vidudu watu wanaopiga simu mjini kuchunguza kitovu cha hela zake. Lililomfikisha hatua ya leo ni kuwa amesikia kuwa kuna wale wanaomkejeli mamake kuwa muuza mboga tu atawezaje kuzaa kiongozi. Lo! Dunia ni hadaa, amesalimu amri!

**Maswali**

(a) Onyesha namna usasa na ukale umejitokeza kwenye kifungu hiki. ***(alama 2)***

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

(b) Fafanua namna swala la kinyume limeendelezwa na mwandishi. (***alama 5)***

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

(c) Thibitisha kuwa jamii hii ina ustaarabu. (***alama 2)***

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

(d) Tambua matatizo manne katika jamii hii. ***(alama 4)***

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………

e) Eleza msamiati ufuatao kama uliyotumika katika kifungu***. (al 2)***

I) kwaheri ya masomo. ………………………………………..

II) amesalimu amri…………………………………………….

2. **MUHTASARI**: (***alama 15)***

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Katika kipindi cha miaka iliyopita, kumekuwa na mfumko wa bei ya bidhaa muhimu hivi kwamba idadi kubwa ya raia wanalala njaa. Uchunguzi uliofanywa na mashirika ya kijamii kuhusu bei ya bidhaa hizo umeonyesha kuwa familia za kawaida zinatumia nusu ya mapato yao kununua chakula. Bila shaka yoyote, hili ni janga linaloendelea kutokota. Tunafahamu kuwa kupanda kwa bei ya petroli kimataifa kumechangia kuongezeka kwa bei hiyo ya vyakula, kwa namna moja au nyingine.

Mbali na vyakula, gharama ya kupanga nyumba, maji, stima na mafuta imepanda kwa muda wa miezi mitatu iliyopita kati ya Desemba na Januari 2017. Kwa mujibu wa Benki ya duniailiyozinduliwa hivi majuzi, kupanda kwa bei ya vyakula kumesukuma familia nyingi katika lindi la umaskini.

Ingawa serikali haina uwezo wa kudhibiti baadhi ya sababu zinazochochea kuongezeka kwa bei ya chakula nchini, haipaswi kutulia tuli ikisubiri suluhisho litokee kisadfa. Inasikitisha kwamba viongozi wetu wanatumia muda mwingi kuchapa siasa huku raia wa kawaida wakiendelea kuumia. Iweje basi katika vikao vyao vya hadhara wanasiasa wanatumia muda mwingi kuzungumzia maswala ya kugawanya wananchi na kufichua njama za kuwaangamiza wapinzani

wao badala ya kueleza namna watakavyokabiliana na janga lililopo la njaa. Ni lini watafahamu kwamba hauwezi kumtawala mtu mwenye njaa?

Kwa muda mrefu, baa la njaa limekuwa likihusishwa na maeneo ya kaskazini mwa nchi yetu; lakini kama uchunguzi ulivyoonyesha, familia nyingi nchini zinaumia na wengi hawawezi kumudu bei ya bidhaa muhimu kama sukari, unga, mafuta ya kupikia na kadhalika.

Wakati umewadia kwa serikali kuchukua hatua madhubuti kwa kuwa kama ilivyo ni vigumu kumtawala mtu aliye na tumbo tupu na ambaye hajijui wala hajitambui kuhusu atakapopata lishe.

(a) Ukizingatia taarifa uliyosoma, fafanua athari za mfumko wa bei kwa wananchi.
(maneno 35 - 40) (Alama 6 1 mtiririko) ***(alama 6)***

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

(b) Eleza mambo muhimu anayoyazungumzia mwandishi katika aya za mwisho nne.
(maneno 60-65) (Alama 8, 1 mtiririko) ***(alama 9)***

**Matayarisho**

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

**3. SARUFI**

A. Andika neno lenye kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya mbele wastani, nazali ya midomo na irabu ya chini kati. (al. 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

B. Bainisha uamilifu wa viambishi katika neno lifuatalo (al 2)

Viliwavyo

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

C. Eleza muundo wa silabi katika neno <u>mbilikimo</u>. (al 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

D. Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi cha A-unganifu, kitenzi kishirikishi kipungufu na kijalizo. (al 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

E. Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi (al 2)

Mwanafunzi huyo akisoma kwa bidii atapita

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

F. Ainisha vihusishi katika sentensi zifuatazo (al 2 )

a) Tunu ni mrembo kama mama yake

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

b) Watawasili kufikia juma lijalo

..........................................................................................................................

.......................................................................................................................................

G. Tambua virai katika sentensi (al 2 )

Wenye bidii kazini wamesifiwa sana bungeni

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

H. Tunga sentensi sahihi ukitumia kiunganishi cha kulinganisha (al 2 )

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

I. Andika katika usemi wa taarifa (al 2 )

"Wanasiasa hawa wenu wakipigana hivi wataharibu nchi" Rais alisema

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

J. Changanua sentensi kwa jedwali (al 4 )

Jirani aliyenisaidia juzi ataondoka mwaka ujao.

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

K. Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo (al 3 )

Alawi alifumiwa mkeka mzuri na shangaziye kwa miyaa

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

L. Tambua aina za vishazi katika sentensi (al 2)

Lazima nile lishe bora ili niwe mwenye afya

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

M. Ainisha sentensi ifuatayo ukitumia vigezo viwili vikuu. (al 2)

Wanafunzi walikuwa wakiamka mapema

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

N. Bainisha maana mbili za sentensi ifuatayo (al 2 )

Mapunda alisema kuwa mkewe amesafiri

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

O. Andika sentensi ifuatayo katika wingi (al 1 )

Onyesha kivumishi katika sentensi ifuatayo

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

P. Geuza sentensi zifuatazo katika nyakati na hali katika mabano (al 2 )

i) Wanafunzi wanafanya mtihani ( ujao hali timilifu)

..............................................................................................................................................

ii) Mtoto amekunywa maziwa (uliopita hali ya kuendelea)

..............................................................................................................................................

Q. Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha miundo miwili ya ngeli ya U-ZI (al 2 )

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

R. Tunga sentensi sahihi yenye kitenzi halisi (al 1 )

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

S. Andika sentensi upya kulingana na maagizo (al 2 )

(i) Miti ilikatwa Nairobi ( tumia viwakilishi vya maneno yaliyopigiwa msitari

..............................................................................................................................................

(ii) Mtoto amekula wali ( geuza katika kauli ya kutendwa)

..............................................................................................................................................

T. Onyesha matumizi ya KI katika sentensi hizi (al 2 )

(i) Hakijapikiwa

..............................................................................................................................................

(ii) Alinunua kimeza hafifu

**4. ISIMUJAMII**

MTU 1: Una shida gani?
MTU 2: Kichwa chaniwanga, tumbo lanisokota na ninahisi uchovu mwingi. Nisaidie tafadhali.
MTU 1: Pole, afya yako itakuwa shwari. Hizi tembe hapa zitakusaidia kupunguza maumivu. Unapaswa kuzitumia mara tatu kwa siku…

(a) (i) Tambua sajili hii ( alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(ii) Kwa kutolea mfano, andika sifa tatu ambazo zingetumika katika sajili hii ( alama 3)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(b) Umepewa jukumu la kuendesha shughuli ya mazishi kijijini mwako. Fafanua sifa tano za lugha utakayotumia wewe na waombolezaji wengine. (alama 5)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

**MINISTRY OF EDUCATION (KNEC COMPLIANT)**

**102/3 KISWAHILI KARATASI YA 3**

**FASIHI**

# THE NAIROBI & CENTRAL REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCKS 2023

**MUDA: Saa 2 ½**

**JINA** ____________________________ **NAMBARI YA MTAHINIWA**________

**SAHIHI**______________ **KIDATO**_____________________

**TAREHE**____________________

**MAAGIZO**

a) Jibu maswali **manne** pekee.

b) Swali la **kwanza** ni la **lazima.**

c) Chagua maswali mengine **matatu** kutoka sehemu **tatu** zilizobaki yaani; Tamthilia,Ushairi na Fasihi Simulizi.

d) Jibu swali **moja** kutoka kila sehemu moja.

e) Kila swali lina alama 20.

f) Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

| Sehemu | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| Ushairi | 20 | |
| Riwaya | 20 | |
| Tamthilia | 20 | |
| Fasihi Simulizi | 20 | |
| Hadithi Fupi | 20 | |
| Jumla | 80 | |


*©2023 The Kenya National Examinations Council*
*Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes*

**1. SEHEMU YA: A USHAIRI**

**LAZIMA**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

SIGOMBEE KIVULIE: Mathias Mnyapala

Ndege akiwa angani, usiseme wangu mie
Mngoje atuwe chini, na ndipo mgombanie
Lakini yupo hewani, tamaa isikwingie
Sigombee kivulie, ndege apaa angani.

Ndege apaa angani, sigombee kivulie
Mnapigana machoni, mwambombea uzurie
Mwalizana kama nyani, matunda mwagombeae
Sigombee kivulie, ndege apaa angani.

Shika awe mkononi, ndipo ukajivunie
Umshikapo mwilini , chukua kajifugie
Kama utavyo moyoni, kufuga ama mwachie
Sigombee kivulie, ndege apaa angani.

Usimlilie nyuni, kwanza akukaribie
Na sauti mdomoni, aimbapo usifie
Saburi ndicho kiini, kila jambo sivamie
Sigombee kivulie, ndege apaa angani.

Mwaingia ushindani, kwa magumi mpanie
Nyinyi nyote ufukani, ndege juu muanie
Ndege atatua lini? Pengine ajiendee
Sigombee kivulie, ndege apaa angani.

Siingie ujingani, majambo mfikirie
Sirukie kifanani, ndege juu muanie
Utafanywa hayawani, jirani wakubeue

Sigombee kivulie, ndege apaa angani.

Atuapo matawini, kwa jicho kuangalie
Awaone dharauni, na mbawa awapigie
Na mate yamo kinywani, katu asiwasogee
Sigombee kivulie, ndege apaa angani.

Kaditama upigani, akheri amuambae
Wawindaji pandaneni, mwachie ndege apae
Lisha aliye tunduni, wajuu sitegemee
Sigombee kivulie, ndege apaa angani.

**Maswali**

a) Eleza dhamira ya shairi hili. (Alama 2)

b)Taja na ufafanue aina mbili za bahari zinazojitokeza katika shairi hili. (Alama 4)

c) Taja na utoe mifano ya mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi hili. (Alama 4)

d) Jadili muundo wa shairi hili. (Alama 4)

e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari /tutumbi. (Alamaa 4)

f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi hili.

i. Nyuni

ii. Saburi

(Alama 2)


©2023 The Kenya National Examinations Council

Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes

**SEHEMU YA B: RIWAYA**

**Chozi La Heri: Assumpta K. Mate**

**Jibu swali la 2 au 3**

2"…umewahi kumwona mtoto wa miaka hamsini ambaye hajasota; sikwambii kusimama?''

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (Alama 4)

b) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika dondoo hili. (Alama 4)

c) Elezea umuhimu wa msemaji katika dondoo hili. (Alama 4)

d) Kwa kutolea mifano mwafaka elezea ufaafu wa anwani 'Chozi La Heri'. (Alama 8)

3."Siasa mbaya maisha mabaya'thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea Riwaya Chozi la Heri . (Alama 20)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA**

**Bembea Ya Maisha: Timothy M. Arege**

Jibu swali la 4 au 5

4"…bado ungali pale pale? Nyumba hii haifuki walau moshi hata kama chakula ni taabu kwako?"

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (Alama 4)

b) Bainisha tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika muktadha huu. (Alama 4)

c) Taja na ueleze sifa mbili za msemewa katika muktadha huu. (Alama 2)

d) Elezea dhamira ya mwandishi katika Tamthilia ya 'Bembea ya Maisha' (Alama10)

5. Jadili namna nafasi ya mwanamke inavyojitokeza/amesawiriwa katika Tamthilia ya 'Bembea ya Maisha'. (Alama 20)

**SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI**

**Jibu swali la 6 au 7**

6 .Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Ewe Mainga wa Ndumi
Siwe uloambia akina mama
Siku tulopinga foleni
Chakula cha msaada kupata
Turudishe vifaranga kwenye miji
Wageuke vijusi tena
Njaa isiwaangamize?

Siwe ulopita
Matusi ukitema
Chumvi na sukari kuturushia ja samadi?
Uhitaji wetu ukatutuma
Kuokota vihela uloturushia
Ukatununua, kura ukapata?
Sasa miaka mitano imetimia
Waja tulaghai tena
Mainga wa Ndumi huna lolote safari hii
Ubunge umekudondoka ukitazama
Wanyonge tumeamua
Kwingine kujaribu

**Maswali**

a) Huu ni wimbo wa aina gani? Kwa nini? (Alama 2)

b) Andika mbinu tatu za lugha zilizotumiwa katika utungo huu huku ukitolea mifano. (Alama 6)

c) Ni nani anayezungumza (nafsineni) katika utungo huu? (Alama 2)

d) Fafanua toni ya utungo huu. (Alama 2)

e) Fafanua umuhimu wa nyimbo za aina hii. (Alama 8)

**7. Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata**.

Ho! Ho! Ho!
Vijana wote tufahamu
Adui katuvamia
Mbiu imeshapigwa!
Sasa unataka kutuangamiza

Karibu wamefika
Akina mama songeni mbnali
Watoto nanyi tokeni
Mchakato utaanza

Vijana wote tushikane
Mikuki tayari tubebe
Mishale nayo tuijaze
Kuirusha, tusiogope
Adui ataangamia

Ho! Ho! Ho!
Vijana mashujaa
Kama mimi ndivyo
Walinda jamii wa leo na kesho
Watamwangamiza adui
Kwa mishale na mikuki
Sisi ni panga!

Tukimaliza udhia nao
Tutasherehekea ushindi
Ushindi wa mashujaa

Vijana tutanguruma kama samba!

**Maswali**

a) Huu ni wimbo wa aina gani? Toa sababu. (Alama 2)

b) Eleza maudhui manne yanayojitokeza katika wimbo huu. (Alama 4)

c) Taja na utoe mifano ya mbinu tatu za lugha zinazojitokeza katika wimbo (Alama 6)

d) Taja sifa tatu za kishairi katika wimbo huu. (Alama 3)

e) Ni mambo yepi ya kuzingatia katika kuainisha nyimbo. (Alama 5)

**SEHEMU E: HADITHI FUPI**

Mapambazuko Ya Machweo na Hadithi

**8.** Kwa kutaja mifano mitano kutoka kwenye hadithi ‘ Fadhila za punda’ eleza ni kwa nini hadithi hii ikapewa anwani hiyo. (Alama 20)

**Jina:................................................ Nambari ya usajili: ....................**

**Sahihi ya Mtahiniwa .............................. Tarehe .....................................**

**KISWAHILI**

**KIDATO CHA NNE**

**MUDA :SAA 2**

# THE NYANZA & WESTERN REGIONS KCSE

# JOINT NATIONAL MOCK 2023

**MAAGIZO**

a. Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima
b. Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia
c. Kila insha isipungue maneno 400
d. Kila insha ina alama 20
e. Kila insha lazima iandikwe ;kwa lugha ya Kiswahili
f. Insha zote sharti ziandikwe katika kijitabu cha majibu ulichopewa

1. Serikali ya Kenya kupitia Wizara ya Elimu imeanzisha mfumo mpya wa elimu ya Umilisi. Mwandikie mhariri wa gazeti la Darubini ukitoa maoni yako kuhusu changamoto zinazotokana na mfumo huu.
2. Utelekezaji wa mtoto wa kiume nchini ni janga kuu. Jadili
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo.
   ``Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe''
4. Anza kwa kifungu kifuatacho.

   ......Hapo ndipo iliponibainikia kuwa nilikuwa nikiogelea baharini pekee

   kinyume na wenzangu wote. (alama 20)


Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes

**MINISTRY OF EDUCATION (KNEC COMPLIANT)**

**JINA………………………………………………DARASA…………………………**

**TAREHE…………………………………………………….**

**KARATASI YA PILI**
**MUHULA WA KWANZA**
**MUDA: SAA 2 ½**

# THE NYANZA & WESTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023

## KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| UFAHAMU | 15 | |
| UFUPISHO | 15 | |
| MATUMIZI YA LUGHA | 40 | |
| ISIMU JAMII | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

## MAAGIZO

- Andikajinalako, nambariyakoyausajili, jina la shulenadarasakatikanafasiulizoachiwahapojuu.
- Tia sahihiyakokishatareheyamtihanikatikanafasiulizoachiwahapojuu.
- Jibumaswaliyote.
- Majibuyoteyaandikwekatikanafasizilizoachwakatikakijitabuhiki cha maswali.
- Majibuyotelazimayaandikwekwalughaya Kiswahili.

## A. UFAHAMU (ALAMA 15)

***Soma kifungukifuatachohalafuujibumaswaliyanayofuata.***

Ikolojianielimuyakisayansiinayohusuuhusianowakimazingirakatiyavituvyenyeuhai (mimeanawanyama) navisivyokuwanauhai( haliyahewaudongoElimuyaikolojiaipokatikamfumowaelimuyamazingira). Mfumohuuumegawanyikakatikasehemumbili: mfumowamazingirayanchikavu, namfumowamazingirayamajini (bahari, maziwa, mitonamadibwi).

Viumbewamejirekebishakulingananamazingirayao. Kwa mfanosamakiwanamatamvuayenyeuwezonakusharabuhewandaniyamaji. Ng’ombewanamapafuyakuvutahewakatikanchikavu. Sehemuzamvuayakawaidazinamajanimaneneiliyawezwkuhifadhimajinyakatizashida. Mimea, wanyama, odongonaviathirivinginevyahaliyahewavinahusianasanakimazingira. Mimeahuotakutegemeahaliyanchi, umbo au surayaardhinaainayaudongo.

Hali yanchiniwastaninahaliyajotoridi, wastaniwamvua, unyevunyevuhewani, upepo, msukumonamwangawamudawamiakathelathini. Duniaimegawanyikakatikakandambalimbali. Kilakandainamimeanawanyamawaainayakekutegemeahaliyanchi. Ukandawaistiwaiunajoto, mvuanaunyevunyevumwingi. Mitiyaukandahuuhufanyamisituminene, yenyemitimirefu. Mitihiinimirefukwasbabuyamsongamanounaofanyamitiigombaniemwangawajuakwakurefuka. Katikamisituhii, ipomimeayakangagainayotambaanakukweamitimingine. Katikaukandawa Savanna, haliyajotonamvuasikubwakamakatikaukandawaistiwai. Kwa sababuhii, sehemunyinginivichakananyikazenyeuwezowakuotanyasizisizohitajimvua.

Upepounafaidanahasarakatikamazingira. Upepohusaidiakusukumamawinguyaletayomvua. Upepounapozidihudhurumimeanawanyamakwasababuhukaushamaliardhini, huvunjanakuharibumimea,

huletavifokwawanyamanapenginekuharibumazingirayawatu. Mimeakatikamazingirahutegemeasananuruyajuailikutengenezachakulachakekiasi cha mwangaupatikanaomahali Fulani huadhirimimeanawanyamawapatikanaokatikamazingirayale.

**Maswali**

***(a)*** Pendekezaanwanikwataarifauliyosoma. ***(alama 1)***

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(b) Elezamaanayaikolojia. (alama 2)

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

***(c)*** Kwa niniwanyamahuwanasifambalimbalizakimaumbile? ***(alama 2)***

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(d) Ni kwavipiukandawaistiwaiunatofautiananaukandawa Savanna? (alama 3)

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(e) Ni kwanamnaganiupepounawezakuwanaatharimbayakwamazingira? (*alama 4)*

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(f) Elezamaanayamsamiatihuukamaulivyotumikakatikakifungu(alama 3)

(i) Matamvua

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(ii) Kusharabuhewa

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(iii) Istiwai

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

***B.*** **Soma taarifaifuatayokishaujibumaswali (*alama 15)***

Chondepulikanikuelezenijuuyamaendeleoyavisiwavyakwetu. Katikakisiwa cha migingowatuwanaishipamojakatikavijiji. Walianzishavijijihivikwaajiliyakuondoadhulumanadhikiya mambo mengiyalazimakwamaisha bora naustawi. Wanaishikwajasholao. Ushirikianondiongaoyamsingiwamaendeleo. Watuwotewakilajanibunakatikavitongojivyakisiwakizimanikamandugu. Wotewanaishikwaumoja. Ubaguziumekwishazikwakatikakaburi la sahau. Wotewanapendakazizaozauvuvi. Hakunaanayepigazohali. Ni aibukwakilamwanakijijikulazadamu. Shibendiyongaoyao. Kilammojaanapiganakwajinonaukuchakujaribukuondoahaliyaunyonge, ufukara, ukosefunahasakuletaharakaiwezekanavyohaliyamaendeleonaustawikwaashabunakisiwa cha migingo.

Viongozinahatawazeewavijijihawaingiliisanavijijihivihataikiwakunatatizokubwa. Hatahivyoviongoziwaserikaliwanaangaliakamawatuwotewanapatachakula bora nahasawatoto, kunywamajisafiilikuepukananamagonjwa, kutoahudumakwaakina mama, watotonakuchukuahatuakadhaazakuendelezaafyayawatukwajumla. Watuwamsalabamwekunduhusaidia mambo kadhanamabwanaafyahushughulikiakuzuiamagonjwayakuambukizakwanjiayakuchanjakama vile ndui, kipindipindunakadhalika.

Watawalawamigingowanatiliamkazokwawatuwazimakuimarishauvuviambaondioutiwamgongowakisiwahikiilikuinuahaliyauvivu, uchuminamaendeleoyakisiwakwajumla.

**Maswali**

***(a)*** Fupishaayaya kwanza kwamaneno 50. (***alama 6, 1 utiririko)***

Matayarisho

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

Jibu

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

***(b)*** Bilakupotezamaanaasilia, andika mambo yotemuhimukutokaayambilizamwisho.(maneno 60) (***alama 7, utiririko 1)***

Matayarisho

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

Jibu

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**C. <u>MATUMIZI YA LUGHA.</u> (*ALAMA 40)***

(a) Kutokananakigezo cha jinsihewainavyozuiliwatajaainambilizakonsonantinautoleemifanokilamoja. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

***(b)*** Fafanuamaanayashadda. (***alama 2)***

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(c) Bainishashamirishokipozinakitondokatikasentesnihii
Babuametengenezewakitikizurinamjukuu wake. (***alama 2)***

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(d) Fafanuatofautiiliyopokatiyakishazinakirai.
***(alama 2)***

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

***(e)*** Hukuukitoleamifanomwafaka, fafanuamajukumuyoyotemanneyaviambishiawali. ***(alama 2)***

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

***(f)*** Undanominodhahaniakutokananakitenzi-abudu. ***(alama 1)***

…………………………………………………………………………………………

***(g)*** Kanushasentensiifuatayo. ***(alama 2)***
Ukionavyaeleavimeundwa

…………………………………………………………………………………………

(h) Nyambuavitenzivifuatavyokatikakaulizilizokwenyemabano. (***alama 2)***

1. Cha (kutendwa)

………………………………………………………………………………………

2. Kosa (kutendesha)

………………………………………………………………………………………

***(i)*** Tungasentensimojakuonyeshamatumizimawiliyakiambishi –ji- (***alama 2)***

………………………………………………………………………………………

***(j)*** Tambuamiundoyoyotemitatuyanominozangeliya LI-YA. ***(alama 3)***

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

***(k)*** Tungasentensiukitumia(***alama 2)***

1. Kihusishi cha ulinganisho

………………………………………………………………………………………

2. Kihisishi cha hasira

………………………………………………………………………………………

l. Changanuasentensiifuatayokwanjiayamatawi. (***alama 4)***

Alifikakishaakaondoka

m. Andikasentensihiikatikahaliyakuamrishawingi. ***(alama 2)***

Ondokahapa.

………………………………………………………………………………………

n. Andikasentensihiikwahaliyaudogowingi. (***alama 2)***

Mtotoamefungamlangowanyumbayao.

………………………………………………………………………………………

o. Yakinishasentensiifuatayokatikawakatiujaohalitimilifu***(alama 2)***

Tamimahakutuzwasikuhiyo.

…………………………………………………………………………………………

p. Andikakinyume. (***alama 2)***

Sufuriailiyoinjikwamekoninichafu.

…………………………………………………………………………………………

q. Andikakatikausemihalisi**.** ***(alama 3)***

Mwalimualinifokeanitokehapomaramoja.

…………………………………………………………………………………………

r. Kaainamaanayaketi. Andikamaanazinginembili. ***(alama 2)***

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**D. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Ninimaanayadhanayausanifishajiwalugha? (***alama 2)***

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(b)NchizaAfrikamasharikiziliundakamatiyalughailikusafirishanakukuza Kiswahili, elezamalengomannemakuunamafanikioyakekatikausanifishaji.

(***alama 8)***

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

**MINISTRY OF EDUCATION (KNEC COMPLIANT)**

# THE NYANZA & WESTERN KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023

## Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

**102/3** **KISWAHILI – FASIHI** **KARATASI YA 3**

**Muda: Saa 2½**

---

**Jina: ………………………………………………Nambari: ……………… Darasa :**

………

**Maagizo**

*a) Andika jina lako, nambari ya usajili, darasa, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*b) Jibu maswali **manne** pekee.*
*c) Swali la kwanza ni la **lazima**.*
*d) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu Tatu zilizobaki Riwaya, Tamthilia na ushairi.*
*e) Unaweza jibu maswali **mawili** kutoka sehemu **moja**.*
*f) Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |


Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes

# SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

### 1. SWALI LA KWANZA (LAZIMA)

Zamani sana Sungura na Fisi walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Mjukuu wangu sijui kama umewahi kuuwazia urafiki wa aina hii, ule wa mmoja wao akijikwaa dole anayeuhisi uchungu wenyewe ni mwenzake.

Siku moja walialikwa karamuni na Tumbili. Marafiki hawa waliafikiana waandamane asubuhi na mapema. Hata hivyo, Fisi alipofika nyumbani kwake moyo wake ulimrai."Ndugu, wewe unajua mambo ya akutanguliaye chanoni hukuzidi tonge na atanguliaye kisimani hunywa maji maenge? Itakuwaje umngojee Sungura na hali kimo chake ndicho hicho? Hata akafika amechelewa atakula shibe yake, wewe unahitaji kutwa nzima kulijaza tumbo lako kuza. Wewe jihimu mapema, huyu mwenzako atakufuata."

Asubuhi na mapema Fisi alishika tariki ... guu mosi, guu pili... guu mosi, guu pili ... hadi kwa Tumbili  Harufu nzuri ya mapochopocho ilihanikiza hewa; harufu ambayo ilimfanya Fisi kuchezesha midomo yake hivi na mate kudondoka ndo ndo ndo! Fisi alifika karamuni na kuchukua nafasi katika viti vya mbele asije akapitwa na chochote.

Nyuma kule Sungura alipitia kwa Fisi lakini hakumpata.

"Lo, kiumbe huyu!" Sungura alimwuliza Fisi kimoyomoyo, "utaacha lini tabia hii ya usaliti?" "Lazima nikukomeshe!"

Sungura alipofika karamuni alikaa kule nyuma akiwazia la kufanya. Fisi ambaye hakuwa na mwao na yaliyokuwa akilini mwa Sungura alimwendea na kumwambia. "Ndugu yangu, mtu huhifadhi akipatacho. Sijui kama nitawahi kuambulia shibe ya aina hii. Je, waonaje tukichukua baadhi ya vyakula hivi tupeleke nyumbani?"

Sungura alimwambia. "Hamna haja kujidhalilisha. Njia mufti ya kuhakikisha hutaona njaa tena ni kuhifadhi kilicho tumboni. Basi nitatumia ujuzi wangu wa utabibu kukusaidia kukitunza chakula tumboni. Fisi alikubali haraka.

Fisi alilia kwa maumivu makali lakini alipofikiria kuhusu kile chakula slivumilia huku mwili mzima unamtetema. Sungura alikamilisha rnpango wake na kutwaa tabasamu la ushindi.

Basi mjukuu wangu, Sungura aliutwaa uzi na sindano ambayo alikuwa kahifadhi kwenye kijaluba akaanza kuupitisha ule uzi polepole kwenye msamba wa fisi. Fisi alilia kwa maumivu makali lakini alipofikiria kuhusu kile chakula alivumilia huku mwili mzima unatetema. Sungura alikamilisha mpango wake na kutwaa tabasamu la ushindi.

Baada ya muda, Fisi alirejea kubugia sahani za vyakula na mifupa bila kufanya nadhari. Polepole, maumbile yalianza kudai haki, naye akatanabahi kwamba Sungura alikuwa kamnyima uwezo wa kuyatosheleza maumbile haja. Aliangaza macho huku na kule, asimwone Sungura. Alijikokota mithili ya ng'ombe anayechungulia kaburi hadi kwa Sungura.

Alimsihi Sungura amwondolee udhia huu lakini Sungura alikataa katakata, akamwambia "Jikune ujipatapo." Na kweli Fisi alijikuna ajipatapo. Kabla Sungura hajafumba jicho, alisikia kilio cha kite, kisha mpasuko mkubwa Sungura aliangua cheko kubwa la stihizai na kumsukuma Fisi kutoka nyumbani kwake huku amefunika mianzi yake ya pua kwa viganja. Huo ukawa mwisho wa urafiki wa Sungura na Fisi. Tangu wakati huo, Fisi yumo mbioni kumtafuta Sungura iii amwadhibu.

Hadithi yangu imeishia hapo. Naomba ng'ombe wangu wafaidi nyasi za kijani na wako wafe kwa kiangazi.

**MASWALI**

(i) Hii ni hadithi ya aina gani? Toa sababu. (alama 2)

(ii)Tambua anayesimuliwa hadithi hii. (alama 1)

(iii) Je, fomyula ya mwisho ina umuhimu gani kwenye hadithi hii? (alama 3)

(iv) Fafanua mbinu zozote ***kumi*** za lugha zilizotumiwa kwenye hadithi. (alama 10)

(v)Taja sababu zinazofanya fasihi simulizi kufifia. (alama 4)

## SEHEMU B: RIWAYA

## CHOZI LA HERI (Assumpta K. Matei)

**2. SWALI LA PILI**

(a) Eleza ufaafu wa anwani **Chozi la Heri** kwa kutolea hoja nane. (alama 8)

(b) **"Hii ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mungu amenifidia yule mwanangu aliyekufa"**

(i) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)

(ii) Tambua sifa ya mnenaji inayoonekana kwenye dondoo. (alama 1)

(iii) Watoto ni viumbe wenye changamoto nyingi. Fafanua ukweli wa kauli hii kwa kurejelea riwaya hii. (alama 7)

**3. SWALI LA TATU**

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yanayofuata.**

"Ni kweli asemavyo Tila," Ridhaa anayarudia maneno haya akilini, "mustakabali wa ukuaji wetu kiuchumi uligonga mwamba wakati sheria ya mkoloni ilipompa Mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zilizotoa mazao mengi. Ukengeushi wa ardhi ukatiliwa muhuri, umilikaji wa ardhi na Waafrika katika sehemu hizi ukapigwa marufuku; si mashamba ya chai, si ya kahawa ... yote yakapata wenyeji wageni ... dau la Mwafrika likagonga jabali. Waafrika, akiwemo baba, Mzee Msubili, walilazimika kuwa, ama vibarua katika mashamba yaliyokuwa yao, au maskwota ambao maisha yao yalitegemea utashi wa Mzungu. Waafrika waliobahatika kuwa na makao yao binafsi walipata sehemu ambazo hazingeweza kutoa mazao yenyewe; na bila shaka hali yao iliweza kutabirika; kuvyazwa kwa tabaka la wakulima wadogowadogo, maskini, wasio na ardhi. Nadhani unaweza kukisia hali ilivyokuwa kwa familia nyingi za Kiafrika. Kama vile Mzee Msubili alivyokuwa akisema, jamii yetu iligeuka kuwa hazina kuu ya wafanyakazi ambamo Wazungu wangeamua kuchukua vibarua kupalilia mazao yao. Vijulanga vilinyakuliwa kwa lazima kutoka kwenye susu zao, hata vifua havijapanuka, vinapelekwa katika maeneo mbalimbali nchini kufanya kazi."

"Hadi sasa hali hii haijabadilika, nakubaliana na Tila," Ridhaa alijiambia. "Ama hii ndiyo ile wanayoiita, *Historical Injustice*?" Ridhaa alimuuliza Tila mawazoni.

**MASWALI**

(a) Changanua mtindo kwenye dondoo. (alama 10)

(b) Jadili sifa zozote **kumi** za Mhusika Ridhaa kwenye riwaya. (alama 10)

## SEHEMU C: USHAIRI

**4. SWALI LA NNE**

**Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata**

Mwanangu, wenye dhambi vishawishi, vikejeli
Mwanangu, katu wasikushawishi, binkuli
Mwanangu, aushi nayo uishi, kama mwali
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, sherati sikuperembe, kakubali
Mwanangu, usiwache wakubembe, kwa sali,
Mwanangu, mithili yao mapembe, ya fahali
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, wajeuri siwe nao, ni shubili
Mwanangu usifwate njia zao, pita mbali
Mwanangu, ujeuri sera yao, mazohali,
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, waongo usiwasifu, kulihali
Mwanangu, uongo ubatilifu, si amali
Mwanangu, ndimi zao hazikifu, si manzili
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, wafisadi siwe nao, kemikali
Mwanangu, tamaa ndo utu wao, si Injili
Mwanangu, wahepe kila uchao, kiakili
Mwanangu sikubali!

Mwanangu, wote walio wabaya, wanadhili
Mwanangu, usije ukawapeya, ikibali
Mwanangu, katika hino duniya, kaa mbali
Mwanangu sikubali!
(J. Kiponda)

a. Fafanua mambo **sita** ambayo yanaweza kuzorotesha maadili ya anayelengwa na shairi hili. (alama 6)
b. Bainisha tamathali **mbili** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili (alama 2)
c. Andika aina **mbili** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
d. Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: (alama 4)
   i. idadi ya vipande katika mishororo.
   ii. mpangilio wa maneno katika mishororo
   iii. idadi ya mizani katika mishororo.
   iv. mpangilio wa vina katika beti.
e. Andika aina **mbili** za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
f. Andika ubeti wa **tano** kwa lugha ya nathari. (alama 4)

**5. SWALI LA TANO**

**A. Mazrui: Chembe Cha Moyo**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Nimeyaandika maneno haya
Kwa niaba ya:
Mamilioni wasio malazi
wabebao vifurushi vilivyo wazi
wazungukao barabarani bila mavazi
...milki yao ya maisha.
Kwa niaba ya:
Maelfu wanouawa bila haki
wiki baada ya wiki

leo sumu au spaki
leo kamba au bunduki
na kwa wale wanosubiri kunyongwa.

Kwa niaba ya:
Vijana walio mitaani
wale mayatima wa maskini
wazungukao mapipani
kila pembe mjini
kuokota sumu kutia tumboni
kujiua bila kujua
ili kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasio jiweza
walao chakula kilichooza
wachukuao choo wakijipakaza
polepole waki jiangamiza
katika vyumba vyao
baridi na giza
kwa sababu hawana watazama
wala wauguza.

Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu
kwa sababu ya madawa tifutifu
yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
Bila ya mtu kuona
kama kwamba sote tu vipofu,

Na kwa niaba yetu sote;
Tuliofungwa vifungoni, duniani
Tuliosukumwa kingoni, maishani
Tuliopokonywa maoni, machoni
Tuliotiliwa sumu, malishoni
Tuliodidimizwa kinyesini
ili ‘maendeleo’
yaendelee kwenda njiani
huku yakitema machicha ya roho zetu.

**MASWALI**

a) "Shairi hili linakatisha tamaa." Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano saba kutoka kwenye shairi. (alama 7)

b) Fafanua umuhimu wa ama mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)

c) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. (alama 3)

(i) tasfida

(ii) kinaya

(iii) tashihisi

d) Eleza kwa kutoa mfano, mbinu moja ambayo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika ubeti wa tano. (alama 2)

e) Andika ubeti wa pill kwa lugha ya nathari. (alama 2)

f) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU D: TAMTHILIA

## BEMBEA YA MAISHA (Timothy Arege)

**6. SWALI LA SITA**

Tambua mandhari yoyote manne na umuhimu wake katika Tamthilia hii.(alama 20)

**7. SWALI LA SABA**

***"Eti la alama! My foot! Eti ameshuka nafasi darasani lakini anapandisha alama…"***

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

b)Eleza maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili.(alama2)

c)Jadili sifa sita za mnenaji.(alama 6)

d)Tathmini umuhimu wa mneneji katika Tamthilia.(alama 8)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

**Jina………………………………………………………Nambari…………………………**

**Shule ……………………………………………Tarehe……………………Sahihi…………**

**102/1**
**Kiswahili**
**Karatasi ya 1**
**Insha**
**MUDA :SAA 1 ¾**

# THE COASTAL & EASTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023

**Maagizo**

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima** kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.
d) Kila insha isipungue maneno 400.
e) Kila insha ina alama 20.
f) Karatasi hii ina kurasa 2 zilizopigwa chapa.
g) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa.
h) Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

***Matumizi ya Mtahini Pekee***

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |


Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes

**MASWALI**

1. Suala la umoja wa kitaifa wakati huu wa kampeni za uchaguzi limekuwa katika vinywa vya wananchi wengi. Andika tahariri katika gazeti la MWANANCHI, kuhusu namna ya kustawisha umoja wa kitaifa.

2. Magonjwa mengi yanasababishwa na mitindo ya kisasa ya maisha. Jadili.

3. Andika insha inayoafiki methali; Asiyejua faida ya mwangaza aingie gizani.

4. Andika insha itakayomalizika kwa; **...** nilipojitazama, nilijidharau kwa aibu niliyopata. Niliapa kutorudia kitendo hicho maishani mwangu.

**MINISTRY OF EDUCATION (KNEC COMPLIANT)**

**Jina:** ________________________________________**Nambari ya Mtahiniwa:** ________________

**Shule:** ______________________________________**Sahihi:** _______________________________

**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**
**Muda: saa 2**

# THE COASTAL & EASTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023

**Maagizo**

i. Andika jina lako na Nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

ii. Weka sahihi yako kisha tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa

iii. Jibu maswali yote.

iv. Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu hiki cha maswali

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

1. **UFAHAMU: (Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

KUKITHIRI kwa visa vya utoaji wa hongo kwa wapiga kura walioshiriki chaguzi ndogo zilizofanyika Jumatatu katika eneobunge la Malindi na Kaunti ya Kericho ni ithibati tosha kuwa ufisadi ume-kita mizizi nchini.Kadhalika,visa hivyo vilidhihirisha kuwa demokrasia imedidimia na taasisi za kupambana na visa vya ufisadi zimefifia.mwezi uliopita, Wakenya kupitia mitandao ya kijamii walishtumu Rais wa Uganda Yoweri Museveni kutokana na kile walichotaja kuwa matumizi ya mabavu' kuhifadhi kiti chake baada ya kuwatishia wapinzani wake.

Watumiaji wa mitandao ya kijamii pia walimkosoa Rais Uhuru Kenyatta kumpongeza wenzake wa Uganda huku wakisema aliunga mkono ukandamizaji wa demokrasia,Lakini, visa vya uhongaji wa wapiga kura vilivyoshuhudiwa katika maeneo ya Malindi na Kericho vikitekelezwa na viongozi wa kisiasa hata Wengine wakiwa wa muungano tawala wa Jubilee, ni dhihirisho tosha kuwa Wakenya hawakuwa na sababu ya kushutumu Rais Museveni.

Utumiaji wa mabavu au kununua wapiga kura ili kushinda uchaguzi ni hujuma kwa demokrasia. Baadhi ya wanasiasa pia wameripotiwa wa kuwa Wanatumia fedha zao kusafirisha watu kutoka eneo moja hadi jingine ili wajiandikishe kuwa wapiga kura na wawachague katika uchaguzi ujao. Huu pia ni ukiukaji wa misingi ya demokrasia.

Ununuaji wa wapiga kura unamanisha mabwanyenye ambao wamehusishwa na sakata mbalimbali za ufisadi ndio nyadhifa mbalimbali za uongozi kwa kuwa wao ndio wana mabunda ya fedha za kuhonga wapiga kura.Viongozi wanaochaguliwa baada ya kuwahonga wapiga kura huwatafanya maendeleo yoyote na badala yake, watakuwa wakihusika na wizi wa rasilimali za umma ili kupata fedha za kuwahonga watu katika uchaguzi unaofuatia. Mabwanyenye hawa wanafanya kila wawezalo kuhakikisha wapiga kura wanaendelea kuzama katika lindi la maskini ili waweze kununuliwa kwa urahisi. Sawa na Esau katika Bibilia tuliyeelezwa kwamba aliuza urithi wake wa kuzaliwa kwa Yakobo kwa kubadilishana na chakula,maskini pia wako tayari kuuza haki yao ya kuchagua kiongozi bora kwa Shilingi mia moja.

Viongozi wanaotoa hongo kwa wapiga kura kwa lengo la kushinda uchaguzi ni ishara kwamba hawana maono wala sera za maendeleo. Badala yake wanang'ang'ania mamlaka ili kujilimbikizia utajiri wala si kusaidia mpiga kura kujiinua kimaisha.

(Taifa leo. Machi 10,2016)

**MASWALI**

(a). Kwa kurejelea kifungu,visa vya kutoa rushwa kwa wapiga kura vinadhihirisha nini? (***Alama 3)***

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(b). Bainisha jinsi nne ambazo viongozi wa kisiasa wanatumia kuendeleza ukiukaji wa misingi ya demokrasia. ***(Alama 4)***

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

c). Fafanua athari za uozo unaorejelewa katika taarifa kwa

(i). Viongozi. ***(alama 2)***

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

(ii). Raia ***(Alama 2)***

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………..

(d). Thibitisha kuwa nyani haoni ngokoye katika muktadha wa Makala haya. ***(Alama.2).***

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(e).Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa (***Alama 2)***

(i). Mitandao ya kijami

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii). Mabwanyeye

………………………………………………………………………………………………….

***2.*** **UFUPISHO *(ALAMA 15)***

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**


*Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes*

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa . Inakera mno kwa vitendo vya kigaidi. Inagadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kwamba magaidi hawa wameelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini, vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na Imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi,manaji,unajisi,ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao. Lakini cha kusikitisha ni kuwa,mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kuhusu kinachoendelea,inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha kwennye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa. Wanaponaswa,hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadhaa na hata kama wanaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika,mbinu hii yanaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani,magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati,polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka Zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

**Maswali**

(a). Ni nini maoni wa mwandishi kuhusu suala la ugaidi. **(alama 7 1 utiririko)** maneno 60-70)

**Nakala chafu**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………………..

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………….……
………………………………………………………………………………………….……
………………………………………………………………………………………….…….
………………………………………………………………………………………….……

(b). Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50 fupisha aya mbili za mwisho. **( Alama 6, 1 utiririko)**

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………………..

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………….……

…………………………………………………………………………………….…………

…………………………………………………………………………………..…………….

……………………………………………………………………………………….……

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

***a.*** Andika sifa zozote mbili za sauti zifuatazo. (***alama 2)***
(i). /u/

……………………………………………………………………………………………………

(ii). /ch/

……………………………………………………………………………………………………

b). Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike muundo wake. (***Alama 2)***
i) igwa

……………………………………………………………………………………………..

ii) Oa

…………………………………………………………………………………………

c). Andika upya sentensi kwa kutumia ‘O’ rejeshi tamati. (***alama 2)***

Gari lililoanguka si lile unalolizungumzia

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

d). Unda nomino kutokana na kivumishi kifuatacho; (***Alama 1)***
Tepetevu

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

(e). Badilisha katika usemi halisi (***alama 3)***

Afisa wa usalama alisema kuwa wangemsaidia ikiwa angeshirikiana nao

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

f). Pambanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha Vishale. ***(Alama 4)***

Letu lililopaliliwa limetuletea mazao mengi.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

g). Ainisha virai vyovyote vitatu ***(Alama 3)***

Mwanafunzi yule mtoro hupenda kutembea katikati ya barabara kila wakati.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(h) Tunga sentensi moja kutofautisha vitate vifuatavyo: ***(Alama 2)***

i) Chaka

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

ii). Shaka

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

j). Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao,hali timilifu (***alama.2)***

Mwanafunzi aliandika insha nzuri

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

k). Andika sentensi hii katika udogo wingi. ***(alama.2)***

Mtoto amefunga mlango wa nyumba yao

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

l). Onyesha matumizi matatu ya alama ya vifungo katika sentensi. ***(alama.3)***


*Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes*

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

m). Eleza maana ya kishazi. ***(Alama 2)***

**…………………………………………………………………………………………………**

**…………………………………………………………………………………………………**

…………………………………………………………………………………………………

n). Nyambua vitenzi vifuatavyo kama ulivyoelekezwa ***(Alama 2)***

i). Suka (kauli ya kutendata)

ii). Pa (kauli ya kutendeka)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

o). Onyesha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo.

Babu alijengewa nyumba kwa mawe na Juma. (***Alama 2)***

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

(p) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo uliyopewa

Mzazi alishangilia matokeo ya mwana. (***alama 2)***

(Anza Mwana…)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

q). Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo.

Mama alinileteа Kanga. ***(alama.2)***

**…………………………………………………………………………………………………**

**…………………………………………………………………………………………………**

r). Yakinisha.

Usiponiita sitaandamana nawe ***(alama.2)***

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

s). Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo.

Mgeni alikuwa amewasili jana. ***(alama 1)***

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**ISIMU JAMII** **(Alama 10)**

(a). Wewe ni mfanyabiashara katika soko la Chapakazi,eleza sifa tano za lugha utakayotumia kuwasiliana na wateja pamoja na washiriki wengine siku ya soko. (***Alama 10)***

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………..

**JINA: ............................................ NAMBARI YAKO: ..........................**

**SAHIHI: ........................................ TAREHE: ...............................**

102/3
KISWAHILI- fasihi
Karatasi 3
MUDA: SAA 2 ½

# THE COASTAL & EASTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023

## HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI- KENYA

**MAAGIZO**
1. Jibu maswali manne pekee
2. Andika majibu yako kwa lugha ya Kiswahili.
3. Swali la kwanza ni la lazima
4. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:- Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi
5. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

**Kwa Matumizi Ya Mtahini Pekee**

| SWALI | UPEO | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| **Jumla** | 80 | |

**1. SEHEMU A: USHAIRI (LAZIMA)**
Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata.

**SIKATE TAMAA**

Umeanguka, inuka, simama kama mnazi
Umechunika, inuka, tia dawa kwa ujuzi
sasa inuka, inuka, kijana ianze kazi
Sikate tamaa

Usife tamaa, nyanyuka, ni muweza wa kutenda
Kuna hadaa, nyanyuka, anza tena kujipinda
Dunia baa, nyanyuka, anza tena kujiunda
Sikate tamaa

Sivunjwe moyo, dunia, hivyo itakunyanyasa
Futa kiliyo, dunia, hiyo idhibiti sasa
Ipe kamiyo, dunia, kamwe, siache kufusa
Sikate tamaa

Una nguvu, simama, wewe upambane nao
Una werevu, simama, uzepuke njama zao
Usiche kovu, simama, ujifunze vumilio
Sikate tamaa

a) Hili ni shairi la aina gani? (al. 1)

b)Onyesha mbinu mbili za lugha katika shairi hili. (al. 4)

c) Eleza muundo wa shairi hili. (al. 4)

d) Tambua idhini ya mshairi. (al. 3)

e) Eleza maudhui ya utungo huu. (al. 2)

f) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nathari. (al. 4)

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (al. 2)
i)baa
ii) kovu

**TAMTHILIA: BEMBEA YA MAISHA- TIMOTHY AREGE**
**Jibu swali la 2 au la 3**
2. Ninasikia jiji lina watu wengi, magari mengi, barabara nyingi, majengo makubwamakubwa tena mengi… Wanasema ukiwa mgeni ni kama msafiri jangwani.

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)


Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes

b) Kwa kutoa mifano, eleza mbinu za lugha zinazojitokeza hapa. (al. 4)

c) Kwa hoja sita, jadili maovu yanayotokea katika jumuiya ya tamthilia Bembea ya Maisha. (al. 12)

3. Lakini maskini mwanangu hatuonani! Ninamwona tu akiwa usingizini. Sisemi naye, sili naye, sichezi naye… Uzazi gani huu sasa?

a) Weka dondoo hili katka muktadha wake (al. 4)

b) Kwa kutoa mifano, eleza mbinu za lugha zinazopatikana kwenye dondoo hili. (al. 4)

c) Maisha ya mwanadamu yamejaa matatizo. Jadili ukirejelea jumuiya ya Tamthilia ya Bembea ya Maisha. (al. 12)

**RIWAYA: CHOZI LA HERI-ASSUMPTA MATEI**
Jibu swali la nne au la tano.

4. Woga huweza kumtia mtu upofu wa muda! Hatimaye moyo wa shauku uliyashurutisha macho kukisoma kile ambacho kilichosomeka kama ujumbe wa mauti.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)

b) Taja na utoe mifano ya mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (al. 4)

c) Fafanua sifa zozote nne za msemaji. (al. 4)

d) Kwa kurejelea riwaya nzima, eleza jinsi tatizo la ukabila/kimbari lilivyoathiri maisha ya wahusika mbalimbali. (al. 8)

5. Hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe. Jadili ukweli wa methali hii kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri. (al. 20)

**HADITHI FUPI**
**MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**

6. Ucha Mungu si kilemba cheupe. Kwa kurejelea hadithi ya Fadhila za Punda, jadili ukweli wa kauli hii. (al. 20)

**7. FASIHI SIMULIZI**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mimi ni mkulima anayesifika
kutoka jimbo hadi jimbo
nishikapo jembe langu
udongo unatetemeka
nipandapo mbegu zangu
huchipuka kwa nguvu za ajabu
mimea yangu kipalilia kwa ustadi usio mfano
wakati wa kuvuna
maghala yangu hufurika
kwa juhudi zangu
mimi ni bingwa wa ukulima
mimi ni shujaa wa ukulima
mimi ndiye mkulima asiye mfano

i)

a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi. (al. 2)

b) Eleza sifa nne za kipera ulichotaja. (al. 4)

c) Taja tamathali mbili za usemi zilizotumika katika kifungu hiki. (al. 4)

ii)

a) Miviga ni nini? (al. 2)

b) Eleza dhima ya miviga. (al. 4)

c) Eleza hasara za miviga. (al. 4)


Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes

JINA: ……………………………………………………SAHIHI: ……………………………

NAMBARI YA USAJILI: …………………………… MKONDO: ………………………………

102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
MUDA: SAA 2

# THE RIFT VALLEY & NORTH EASTERN

# REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023

**Maagizo**

a) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima**.*
b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
c) *Kila insha isipungue maneno **400.***
d) *Kila insha ina alama 20.*
e) *Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya **Kiswahili.***
f) *Insha zote **sharti** ziandikwe katika nafasi ulizoachiwa kwenye kijitabu hiki cha maswali.*
g) ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| Jumla | 40 | |

1. Lazima:

   Wewe ni mwakilishi wa vijana katika gatuzi lenu. Kumekuwa na tuhuma za vijana kutumia vibaya simu tamba katika jamii. Andika mahojiano yako na mwanahabari ukitetea namna simu tamba inavyowafaidi vijana.

2. Fafanua umuhimu wa kudumisha amani nchini wakati wa kampeni na uchaguzi wa kisiasa.

3. Andika insha inayooana na methali ***mchuma janga hula na wa kwao.***

4. Andika insha itakayoisha kwa maneno yafuatayo:
   ….nilipogutuka niliangaza macho huku na kule. Aah! Kumbe nilikuwa nikiota!

**JINA.........................................NAMBARI YA USAJILI........DARASA...........**

**102/2**
**KISWAHILI LUGHA**
**KARATASI YA PILI**
**MUDA:SAA 2**

# THE RIFT VALLEY & NORTH EASTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023

**Maagizo**

*(a)Andika jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*(b)Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

*(c) Jibu maswali yote.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

## 1 UFAHAMU (*alama 15)*

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishanji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano bainaya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huuhautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu;tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi,kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi na kudumisha uhusiano wetuwa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu,unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili,mahusiano ya kipindi cha wastani,kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi,washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekanakudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya,hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii waoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri,uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe,kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoaukuta wauhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano katiya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wamajirani. Vimbunga

vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasahuweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujirikatika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani,  kwenye sehemu za ibada,kwenye kituo cha mafuta,kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekanowa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na'uhusiano wa chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha  kuwa kinachoshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea,nguo anazokufulia,ususi anokufanyia na kadhalika. Mahussiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzakekwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula,amefutwa kazi,amefiliwa,ameibiwa  na kadhalika.
Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusianavipi na jamaa zetu, marafiki zetuna majirani zetu? Je, uhusianowetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

*(a)* Taja kigezo cha kuzungumzia mahusiano. ***(alama 1)***

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

*(b)* Eleza imani ya watu kuhusu mahusiano ya watu. ***(alama 1)***

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

*(c)* Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (***alama 2)***

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................


*Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes*

*(d)* Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo.(***alama 2)***

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

*(e)* Taja sifa kuu za mahusiano ya muda mfupi. ***(alama2)***

....................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

*(f)* Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? ***(alama2)***

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

*(g)* Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. ***(alama 3)***

(i) inasigana.............................................................................................................................

(ii)yameghoshi…………………………………………………………………………………………………………….

(iii)vighairi………………………………………………………………………………………………………………

## 2 UFUPISHO *(alama 15)*

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwauchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea uwezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha, kuyatawalana kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanawezakuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu huweza kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishswa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano,kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambabmba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', ' mjanja', 'hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kunifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu,ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kuthibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapomfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe,ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a ) Fupisha aya ya pilina tatu (maneno 55-60)(alama 5, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................


*Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes*

**Nakala safi**

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane. (maneno 100-110) (***alama 10, 2 za utiririko)***

**Matayarisho**

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………


*©2023 The Kenya National Examinations Council*

*Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes*

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

## 3 MATUMIZI YA LUGHA (*alama 40)*

***(a)*** Taja sauti mbili zinazotamkwa mdomoni.
***(alama 2)***

…………………………………………………………………………………………………………………………

***(b)*** Andika visawe vya maneno yafuatayo; (***alama 2)***
i)doa……………………………………………………………………………………………………………………
ii)omba.........................................................................................................................

(c ) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ***(alama 2)***

Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo .

…………………………………………………………………………………………………………………………

(d) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo;

Hawa ni watoto wa marehemu Bwana Ndovu na Bi.Makombo……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………

***(alama 2 )***

…………………………………………………………………………………………………………………………

(e) Eleza matumizi ya alama ya ritifaa kwa neno lifuatalo;

N'shamchukua ***(alama 2)***

…………………………………………………………………………………………………………………………

(f) Eleza mofimu katika neno lifuatalo ***(alama 3)***

Walichokilalia

..........................................................................................................................................

(g) Bainisha vitenzi vilivyo katika sentensi ifuatayo: ***(alama 2)***

Kalamu aliyokuwa nayo mwalimu ni ya mwanafunzi.

..........................................................................................................................................

(h) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale ***(alama 4)***

Chakula kitamu kimeandaliwa.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(i)Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha matumizi matatu ya kinyota katika sentensi. (***alama 3)***

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(j)Tunga sentensi moja ukitumia kielezi cha wakati na kielezi cha mahali. ***(alama2)***

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(k) Toa mfano wa neno lenye muundo ufuatao wa silabi. ***(alama 1)***

IK+KI+KI+KI

..........................................................................................................................................

(l) Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo. ***(alama 2)***

(i) kibainishi

.................................................................................................................................................

(ii)parandesi

.................................................................................................................................................

(m) Tumia neno –baya kama: (***alama 2)***

(i) kiwakilishi

.................................................................................................................................................

(ii)kielezi

.................................................................................................................................................

(n) Tunga sentensi sahili ukitumia kitenzi 'la' katika kauli ya tendewa. ***(alama 2)***

.................................................................................................................................................

(o)Unganisha sentensi zifuatazo ukitumia neno japo;

i)Selina alijitahidi sana.

ii)Selina hakushinda mbio hizo.

.................................................................................................................................................

(p)Kwa kuzingatia maagizo andika upya sentensi ifuatayo: (***alama2)***

Tinga amewafanya ng'ombe wake wanywe maji.

(Anza kwa : Mifugo wangu …………..usitumie 'amewafanya')

.........................................................................................................................................

(q)Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na kivumishi kimilikishi.
(alama 2 )

.........................................................................................................................................

(r) Bainisha maana mbili zinazojitokeza kutokana na sentensi hii. ***(alama 2)***

Umu alimwandikisha mkewe.

.................................................................................................................................

(s)Onyesha dhamira ya sentensi hii; ***(alama 1)***

Huenda mvua ikanyesha leo

...........................................................................................

## 4.ISIMUJAMII ***(Alama 10)***

Kumekuwa na mijadala mingi kuhusu athari ya chanjo dhidi ya ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Kovid-19.Wewe ni Afisa wa afya katika eneo lenu umealikwa kutoa hotuba kuhusu usalama wa chanjo hii .Eleza sifa kumi za lugha utakayotumia.

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………


Contact Kenya Educators 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 for Marking Schemes

MINISTRY OF EDUCATION (KNEC COMPLIANT)

# THE RIFT VALLEY & NORTH EASTERN REGIONS KCSE JOINT NATIONAL MOCK 2023

**KIDATO CHA NNE**

**KARATASI YA TATU (102/3)**

**MUDA: SAA 2 ½**

**JINA: .......................................................................... SAHIHI: ...........................................**

**NAMBARI YA USAJILI: ................................ MKONDO: ……………...…....................**

**MAAGIZO:**

a. Swali la kwanza ni la lazima
b. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
c. Jibu jumla ya maswali manne
d. Kila swali ni alama 20
e. Tumia lugha ya Kiswahili

**SEHEMU YA A: USHAIRI (ALAMA 20)**

**Swali la lazima**

**Soma shairi kisha ujibu maswali**

Angawa mdogo dagaa, amekomaa
Kaanga kidogo, atakufaa
Kalia kinaya, h'ondoa njaa

Wa kwako udogo, kijana sio balaa
Na sio mzigo ,kijana bado wafaa
Toka kwa mtego ,kijana sinyanyapaa

Nasaha kidogo, kijana ukubwa jaa
Jikaze kimbogo, kijana wacha kukaa
Chimbua mhogo, kijana usibung'aa

Na wake udogo, dagaa hajambaa

Kuliko vigogo ,dagaa hajambaa

Hapati kipigo ,dagaa hauna fazaa

Maisha si mwigo, kijana ushike taa

Sihofu magego. Kijana nawe wafaa

Kazana kidogo, kijana kugagaa

Maswali

a)Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama 2)

b)Eleza arudhi zilizofuatwa katika shairi hili (alama 4)

c)Onyesha jinsi malenga alivyotumia uhuru wake. (alama 3)

d)Tambua bahari katik shairi hili kwa kutegemea;

i)Vipande vya mishororo

ii)Mpangilio wa vina

iii)Idadi ya mishororo (alama 3)

e)Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 3)

f)Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika shairi.(alama 3)

g)Eleza toni ya shairi hili (alama 2)

**SEHEMU YA B: RIWAYA YA CHOZI LA HERI NA ASUMPTA MATEI**

2. Athari ya vita katika nchi ya Wahafidhina ni kioo cha bara ya Afrika. Jadili(alama 20)

AU

3. Riwaya ya Chozi la heri imejaa aina mbalimabli za migogoro.Jadili(alama 20)

**SEHEMU YA C: HADITHI YA MAPAMBAZUKO NA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**

4.”Ondoa wasiwasi mhibaka ,***you are in very safe hands*** .Usiulize maswali , its okay. Tulikuja sote jana baada ya ***dance*** , umesahau hivi?’

i) Fafanua muktadha wa dondoo hili.(alama 4)

ii) Taja na ueleze mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo.(alama 4)

iii) Jadili madhara ya pombe katika jamii kama inavyodhihirika katika hadithi ya Kila mchezea wembe. (alama 12)

Au

5. Eleza matatizo yanayomkumba mtoto wa kike kwa mujibu wa hadithi ya Sabina.(alama 20)

**SEHEMU YA YA D: TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA NA TIMOTHY AREGE**

6. Tambua nafasi ya mwanamke jinsi alivyoshughlikiwa na mwandishi katika Tamthilia hii..(alama 20)

AU

7. 'Ulimwengu umeendelea sana"

a)Weka dondoo katika muktadha wake. (alama 4)

b) Fafanua sifa sita za msemaji.(alama 6)

c)Eleza kwa nini huku kwa msemaji hakujaendelea.(alama 10)

**SEHEMUA YA E: FASIHI SIMULIZI**

8.a)Taja na ufafanue hatua zozote nne za utafiti nyanjani kwa mfuatano wake.(alama 8)

b)Tambua baadhi ya changamoto ambazo mtafiti anaweza kumbana nazo akiwa nyanjani(alama 8)

c) Data iliyohifadhiwa kwa njia ya maandishi inafisha vipi uhalisia wa Fasihi simulizi?(alama 4)

***Mwisho***